**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**621** **KISWAHILI**

**Muda: Saa 3.** **Jumatatu, 02 Mei 2005 mchana**

---

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu **B** and **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Taja mambo manne ya kuzingatia mwalimu anapochagua mbinu ya kufundishia.
2. Eleza kwa mifano tofauti kati ya shairi na methali.
3. Toa hoja nne zinazothibitisha umuhimu wa barua za magazetini kwa jamii.
4. Bainisha hatua nne ambazo mwanafunzi anafuata kusikiliza na kuelewa hotuba.
5. Eleza tofauti kati ya muhtasari wa Kiswahili na mtaala wa elimu.
6. Toa hoja nne kuthibitisha umuhimu wa nyimbo katika malezi ya watoto.
7. Eleza sifa nne za insha bora.
8. Bainisha faida nne za mwalimu kutumia vitabu vya rejea katika ufundishaji.
9. Taja mambo manne yanayoweza kujitokeza katika mwongozo wa usahihishaji.
10. Eleza umuhimu wa kuandika shajara ya kazi kwa mwalimu wa Kiswahili.

**SEHEMU B (Alama 30)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. Kwa hoja tano, eleza nafasi ya maswali na majibu katika kukuza fikra za wanafunzi.
12. Jadili hatua nne za mchakato wa ujifunzaji wa Kiswahili.
13. Kwa hoja tano, thibitisha kuwa vitendawili ni sehemu ya urithi wa Kiswahili.
14. Eleza sifa tano za mwandishi bora wa insha.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

15. Eleza sifa tano za zana bora za kufundishia.

16. Toa faida tano za mitihani kwa mwalimu na mwanafunzi.

17. Jadili mbinu tano zinazoongeza ushirikiano wa wanafunzi darasani.

18. Eleza changamoto tano za kutumia mbinu ya ziara katika ufundishaji.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org